

# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

## WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO



### TAMKO KUHUSU HATUA ZA KUJIKINGA DHIDI YA TISHIO LA WIMBI LA NNE LA MAAMBUKIZI YA UGONJWA WA UVIKO-19 NCHINI.

**Tarehe 27 Novemba, 2021 Dodoma**

**Ndugu Wananchi,** Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto imekuwa ikitoa taarifa kwa wananchi mara kwa mara kuhusiana na mwenendo wa magonjwa, yakiwemo yale ya mlipuko pamoja na hatua zinazochukuliwa kuzuia na kudhibiti magonjwa hayo. Wote tumeshuhudia Dunia ikipambana na mlipuko wa ugonjwa wa UVIKO-19. Nchi mbalimbali zimeendelea kuchukua hatua za kukabiliana na hata kupunguza visa vipya. Hata hivyo kumekuwa na wimbi la pili na la tatu la mlipuko wa ugonjwa huo, ambapo nchi nyingi zimeathiriwa ikiwemo Tanzania. Hivi karibuni kumekuwa na tishio la kutokea wimbi la nne kutokana na viashiria vifuatavyo;

- Taarifa za ongezeko la visa vipya na anuai mpya ya virusi hivi katika baadhi ya nchi duniani.
- Kuwepo kwa wasafiri wengi ndani na nje ya nchi katika kipindi hiki cha sikukuu za mwisho wa mwaka,
- Asilimia ndogo ya watu waliochanja nchini

**Ndugu Wananchi,** Hadi kufikia tarehe 26 Novemba, 2021 jumla ya wagonjwa **259,502,031** na vifo **5,183,003** vimetolewa taarifa Duniani. Tangu kuripotiwa kwa ugonjwa huu hapa nchini tarehe 16 Machi, 2020 hadi tarehe 19 Novemba, 2021, jumla ya wagonjwa **26,261** na vifo **730** vilitolewa taarifa.

Kwa ujumla maambukizi yameanza kuongezeka duniani na baadhi ya nchi zinaviashiria vya uwepo wa wimbi la nne la maambukizi ya ugonjwa


wa UVIKO 19. Aidha, taarifa ya Shirika la Afya Duniani ya tarehe 26 Novemba, 2021, iliripoti kuwa kuna anuai mpya ya kirusi cha UVIKO 19, kiitwacho **Omicron, kinachosemekana kuwa na uwezo wa kusambaa haraka**. Kutokana na hali hii hatuna budi kuendelea kuchukua hatua sahihi za kujikinga dhidi ya ugonjwa huu.

**Ndugu Wananchi**, Wizara inasisitiza kuendelea kuchukua tahadhari ili kujikinga na tishio la wimbi la nne la ugonjwa wa UVIKO-19 zikiwemo;

- a. Kuendelea kujitokeza kupata chanjo ya UVIKO 19 ambayo inatolewa bure kwenye vituo vya kutolea huduma za afya kote nchini. Aidha, Chanjo zimeonyesha ufanisi mkubwa dhidi ya madhara ya UVIKO-19,
- b. Uvaaji wa barakoa, kunawa mikono kwa maji tiririka na sabuni au kutumia vipukusi, kufanya mazoezi na kutumia tiba asili zinazoshauriwa na wataalamu.
- c. Kuendelea kuepuka mikusanyiko isiyo ya lazima,
- d. Kila sekta kuendelea kutekeleza miongozo ya kujikinga na UVIKO 19 katika maeneo yao,
- e. Kuimarisha uchunguzi wa wasafiri katika viwanja vya ndege, bandari na mipaka ya nchi kavu,
- f. Kufanya ufuatiliaji wa nchi zenye ongezeko la wagonjwa na kuchukua hatua stahiki.

**Ndugu Wananchi**, Nawasihi, mueendeleee na shughuli za uzalishaji mali kwa kuchukua tahadhari kama zilivyoainishwa hapo juu. Aidha, Wizara inaendelea kufuatilia mwenendo wa anuai mpya ya UVIKO 19 ikiwemo Omicron na kufanya tathmini ya kina ya hatua madhubuti za kuchukua ili kukabiliana na kuzuia wimbi la nne. Wizara itaendelea kutoa taarifa kwa umma kuhusu mwenendo wa magonjwa ya milipuko nchini mara kwa mara. **Mwisho, Nawaomba wananchi muendeleee kufuatilia na kuzingatia taarifa kutoka vyanzo rasmi.**

**Imetolewa na;**

  
Dkt. Aifello W. Sichaabwe  
**Mganga Mkuu wa Serikali**